VOLUME V

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA MBUNGE, JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

## UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (2020—2025)

## TAARIFA YA MWAKA WA FEDHA 2023/2022
## VOLUME V

**JUNI 30, 2023**

**YALIYOMO**


1. YALIYOMO……………………...……………...1

2. UTANGULIZI…………………………………….. 2

3. MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) YA MWAKA 2020-2025
*(TAARIFA YA MWAKA WA FEDHA 2023/2022)*

3.1 MIRADI YA ELIMU………………………….  5

3.2 MIRADI YA AFYA…………………………….. 37

3.3 MIRADI YA KILIMO, UVUVI NA UFUGAJI…. 43

3.4 MIRADI YA MAJI……………………………….. 51

3.5 MIRADI YA UJENZI WA BARABARA……….. 63

4. MENGINEYO…………………………………. 69

5. HITIMISHO……………………………………….  80

6. SHUKRANI……………………………………. 82

## UTANGULIZI

Kitabu hiki ni moja ya chapisho linalotoa taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini kuanzia Mwaka 2020 hadi 2025

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, ameweka utaratibu wa kuchapisha vitabu vinavyoelezea mafanikio ya utekelezaji wa Ilani za Uchaguzi za CCM ndani ya Jimbo lao kama ifuatavyo:

**Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015-2020:**

Vitabu viwili (2) vilichapishwa:
(i) Julai 7, 2019 (Volume I)
(ii) June 30, 2020 (Volume II)

**Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025:**

Machapisho ya utekelezaji wa Ilani hii ya Uchaguzi yameanza kuchapishwa kwenye vitabu kama ifuatavyo:
(iii) Juni 30, 2021 (Volume III)
(iv) Juni 30, 2022 (Volume IV)
(v) Juni 30, 2023 (Volume V)
(vi) Juni 30, 2024 (Volume VI)

Jimbo la Musoma Vijijini lina jumla ya Kata 21 zenye Vijiji 68 na Vitongoji 374. Jimbo letu limechagua vipaumbele vitano kutoka ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025.

Vipaumbele hivyo ni: (i) Elimu, (ii) Afya, (iii) Kilimo, Uvuvi na Ufugaji, (iv) Tabianchi na Mazingira, na (v) Michezo na Utamaduni.

Maji, umeme, barabara, vyombo vya usafirishaji na mawasiliano, rasilimali watu, na taasisi za fedha na uchumi ni nyenzo muhimu zinazohitajika kufanikisha utekelezaji wa miradi inayoibuliwa kutoka kwenye vipaumbele vyetu vitano.

Wanavijiji kwa kushirikiana na viongozi wao wa ngazi mbalimbali hupendekeza miradi ya maendeleo inayokidhi mahitaji yao, na huchangia nguvukazi na mali zao kwenye utekelezaji wa miradi ya chaguo lao. Uanzishwaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wanavijiji unafuata taratibu na sheria zilizowekwa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan inapongezwa sana na wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini kwa kuendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoendelea kuboresha na kuimarisha uchumi na ustawi wa wananchi wa Jimbo hili.

Kitabu hiki (Volume V) ni chapisho linaloelezea utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini kwa kipindi cha mwaka mmoja wa fedha (30 Juni 2023 - 1 Julai 2022). Vilevile, taarifa hii inaonesha michango mingi na mikubwa iliyotolewa na Serikali Kuu, Mbunge wa Jimbo, Wanavijiji, baadhi ya Wazaliwa wa Jimboni mwetu, na Wadau wengine wa maendeleo ya Musoma Vijijini.

Kitabu hiki, kama vilivyo vingine vyote vya taarifa za maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini hugawiwa bure. Haviuzwi!

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA ELIMU

**(30 Juni 2023 – 1 Julai 2022)**

## SERIKALI YATOA MCHANGO MKUBWA WA TSH MILIONI 573 KWENYE UJENZI WA WANYERE SEKONDARI

*June 9, 2023*



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo akiwa na Wanakijiji kwenye Mkutano uliofanyika jana Kijijini hapo kwenye eneo la ujenzi wa Sekondari mpya, ambayo inajengwa ndani ya Kitongoji cha Mwikoro, Kijijini Wanyere, Kata ya Suguti, Musoma Vijijini.*

Jimbo la Musoma Vijijini laendelea kutatua matatizo yanayowakabili wanafunzi wanaosoma kwenye Sekondari za Kata za Jimboni humo.

**Matatizo makuu yanayowakabili ni:**
*Umbali mrefu wa kutembea kwenda masomoni
*Mirundikano ya wanafunzi madarasani
*Upungufu au ukosefu wa maabara za masomo ya sayansi
*Ukosefu wa maktaba
*Upungufu mkubwa wa walimu, hasa wa masomo ya Sayansi na Lugha

**Ujenzi wa Sekondari mpya Kijijini Wanyere:**
Kijiji cha Wanyere ni moja ya vijiji vinne (Chirorwe, Kusenyi, Suguti na Wanyere) vya Kata ya Suguti yenye Sekondari moja iliyoko Kijijini Suguti

Wanafunzi wa Kijiji cha Wanyere wanalazimika kutembea zaidi ya KILOMITA 30 kwenda na kurudi kutoka masomoni kwenye Sekondari yao ya Kata. Baadhi ya wanafunzi wamepanga vyumba (na wanajipikia) karibu na eneo la shule hiyo.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo alitembelea Kijiji cha Wanyere kwa malengo makuu mawili:
*Kupokea kero za Wanakijiji na kuzitatua
*Kuhamasisha ujenzi wa sekondari mpya kijijini hapo.

**Michango ya ujenzi wa Wanyere Sekondari:**
Mbunge Prof Muhongo aliendesha HARAMBEE ya kuanza ujenzi huo na michango iliyotolewa ni kama ifuatavyo:

**Wanakijiji wa Wanyere wameanza kuchangia:**
*Nguvukazi za kusomba mchanga, mawe, maji na kuchimba msingi wa jengo moja la madarasa 2 na ofisi 1 ya walimu
*Fedha taslimu takribani Tsh milioni 2.5

**Wanakijiji wa Kataryo:**
*Saruji Mifuko 30 imetolewa na Kijiji jirani cha Kataryo cha Kata jirani ya Tegeruka. Watoto wa Kijiji hiki jirani wanasoma Kijijini Wanyere.

**Mbunge wa Jimbo:**
*Saruji Mifuko 100 - Prof Muhongo ameanza kutoa michango yake kwa kuchangia saruji hiyo.

**Halmashauri yetu (Musoma DC):**
*Bado haijatoa mchango wowote!

**Serikali Kuu (TAMISEMI):**
Bajeti ya Mwaka 2023/2024, Serikali itatoa Tsh Milioni 573 kupitia Mradi wake wa SEQUIP kwa ajili ya ujenzi wa Sekondari mpya Kijijini Wanyere. Hii itakuwa Sekondari ya pili ya Kata ya Suguti.

Wananchi na Viongozi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanaishukuru Serikali, chini ya uongozi mzuri wa Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuongeza ubora wa utoaji wa elimu Jimboni mwao.

Usisahau kutembelea TOVUTI ya Jimbo letu ambayo ni:
www.musomavijijini.or.tz

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## KIJIJI CHA NYASAUNGU CHADHAMIRIA KUFUNGUA SEKONDARI YAKE JANUARI 2024

*June 2, 2023*



*Kikao cha Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini na Wananchi wa Kijiji cha Nyasaungu, Kata ya Ifulifu Musoma Vijijini.*

Leo, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo, ametembelea Kijiji cha Nyasaungu, Kata ya Ifulifu kwa lengo la kutathimini utekelezaji wa miradi yao ya maendeleo.

**Miradi inayotekelezwa Kijijini hapo ni ya:**
*Ujenzi wa Sekondari
*Ujenzi wa Zahanati
*Uboreshaji wa miundombinu ya elimu kwenye shule yao ya msingi (S/M Nyasaungu)

Kero zilizotolewa na kupata majibu kutoka kwa Mbunge huyo ni kuhusu upungufu mkubwa kwenye upatikanaji wa:
*Maji
*Umeme
*Chakula (ukame)
*Walimu wa S/M Nyasaungu
*Nyasaungu Sekondari

Kata ya Ifulifu haikuwa na Sekondari yake, na inashukuru Serikali kuchangia kwa kiasi kikubwa sana ujenzi wa Sekondari ya Kata (Ifulifu Sekondari), Kijijini Kabegi.

Kijiji cha Nyasaungu ni moja ya vijiji vitatu vya Kata ya Ifulifu. Kijiji hiki kiko pembezoni na mbali na vijiji vingine vya Kata hii. Vilevile, jiografia yake (mito, vichaka, n.k.) inakifanya kuwa na ugumu wa kufikika, hasa wakati wa mvua - mazingira haya ni hatarishi kwa wanafunzi.

**Ujenzi wa Nyasaungu Sekondari umeanza kwa kutumia michango ya:**

*Wanakijiji
*Mbunge wa Jimbo
*Mfuko wa Jimbo

Halmashauri inaombwa ianze kuchangia ujenzi wa Sekondari hii ambayo watumiaji wake wengi watakuwa watoto wa wafugaji wa Kijiji cha Nyasaungu.

Nyasaungu Sekondari kufunguliwa Januari 2024

**Ujenzi umefikia hatua ya kukamilisha:**
*Vyumba 3 vya Madarasa
*Choo cha Matundu 6
*Jengo la Utawala

**Michango ya Mbunge wa Jimbo**
Mbunge wa Jimbo ataendelea kuchangia ujenzi huu kama alivyofanya hapo awali.

Wanakijiji wameamua kuendelea na ujenzi wa Sekondari yao kuanzia tarehe 10.6.2023. Wakianza ujenzi tarehe hiyo Mbunge huyo atawachangia saruji na mabati.

**Kwa sasa, Jimbo letu linajenga Sekondari nne (4) mpya, ambazo ni:**
*Nyasaungu Sekondari
(Kata ya Ifulifu, sekondari ya pili ya Kata)

*Muhoji Sekondari
(Kata ya Bugwema, sekondari ya pili ya Kata)

*Wanyere Sekondari
(Kata ya Suguti, sekondari ya pili ya Kata)

*Sekondari ya Kisiwa cha Rukuba
(Kata ya Etaro, sekondari ya pili ya Kata)

Jimbo letu lenye Kata 21 zenye Vijiji 68 na Vitongoji 374, lina jumla ya Sekondari 27 (25 za Kata, na 2 za binafsi)

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## SEKONDARI ZA KATA ZAENDELEA KUJENGA MAABARA ZA MASOMO YA SAYANSI

April 25, 2023



*Ujenzi wa Maabara 3 (Physics, Chemistry & Biology) za Mtiro Sekondari ya Kata ya Bukumi, Musoma Vijijini.*

Jimbo la Musoma Vijijini lenye Kata 21 lina Sekondari za Kata 25 na za Binafsi 2.

Jimbo hili limeamua kujenga Maabara 3 za Masomo ya Sayansi kwenye kila Sekondari ya Kata. Maabara hizo ni za Physics, Chemistry & Biology.

Sekondari 3 tu kati ya 25 ndizo zina maabara 3, nyingine zinazo mbili au moja.

Sekondari mpya zinazoendelea kujengwa na Wanavijiji lazima ziwe na maabara hizo.

Imeamuliwa kwamba, Fedha zote za Mfuko wa Jimbo, zinatumika kwenye ujenzi wa maabara tatu za masomo ya sayansi kwenye sekondari za Kata.

**Mtiro Sekondari**
*Sekondari ya Kata ya Bukumi yenye Vijiji 4 (Buira, Bukumi, Buraga & Busekera)

*Ilifunguliwa Mwaka 2006
Haina maabara hata moja

**Wanafunzi wa Mtiro Sekondari**
*Jumla ya Wanafunzi ni 681
*Jumla ya Walimu wa ajira ya Serikali ni 13, na 4 ni Walimu wa muda (kujitolea) wanaopewa posho kutoka kwa Wazazi wenye watoto shuleni hapo.

**Mwitikio wa Masomo ya Sayansi**
*Walimu wanaofundisha Masomo ya Sayansi ni wanne (4)
*Walimu wanaofundisha Hisabati (Maths) ni wawili (2)

**Jumla ya Wanafunzi wa Form III ni 110**
*14 wanasoma Physics
*17 wanasoma Chemistry
*110 wanasoma Biology (kwa kulazimika)

**Jumla ya Wanafunzi wa Form IV ni 123**
*21 wanasoma Physics
*26 wanasoma Chemistry
*123 wanasoma Biology (kwa kulazimika)

## UMUHIMU WA KUWEPO MAABARA KWENYE SEKONDARI

*Takwimu hizo hapo juu zinaonesha mwitikio mdogo sana wa wanafunzi wetu kupenda kusoma Masomo ya Sayansi

*Kuwepo kwa Maabara za Masomo ya Sayansi ni muhimu kwa kufundishia (Walimu) na kwa kujifunza, hasa kwa vitendo (Wanafunzi)

## MTIRO SEKONDARI WANAJENGA MAABARA 3 ZA MASOMO YA SAYANSI

Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo, alipiga Harambee ya ujenzi wa Maabara 3 za Masomo ya Sayansi, na matokeo ni MICHANGO ifuatayo:

**Wanavijiji wa Vijiji 4**
(Michango inaendelea kutolewa)
*Nguvukazi ya kuchimba misingi
*Mchanga trip 27
*Kokoto trip 2
*Saruji Mifuko 8
*Fedha taslimu Tsh 1,508,000
*Wazaliwa wa Kata ya Bukumi & Wadau wengine
Tsh 1,500,000

**Mbunge wa Jimbo**
*Saruji Mifuko 150 (ameanza kwa kutoa 75)

**Mfuko wa Jimbo**
(Mwenyekiti, Mbunge wa Jimbo)
*Saruji Mifuko 200
*Nondo 49

## MAOMBI KUTOKA KWA WANANCHI WA MUSOMA VIJIJINI

Halmashauri yetu (Musoma DC) ianze kuchangia ujenzi wa Maabara za Masomo ya Sayasi kwenye Sekondari zake za Kata, isusibiri kufanya kazi ya kuratibu fedha zinazotolewa na Serikali Kuu!

*Wazaliwa wa Musoma Vijijini waanze au waendelee kuchangia Sekondari za Kata za kwao kwenye ujenzi wa Maabara za Masomo ya Sayansi, na Maktaba.

**SAYANSI NI KILA KITU**

**UCHUMI WA KISASA UNAHITAJI SAYANSI**

**MAFANIKIO MAKUBWA YA KIUCHUMI YA CHINA, INDIA & BRAZIL YANAENDANA NA UWEKEZAJI MKUBWA KWENYE SAYANSI**

*Ofisi ya Mbunge*
*Jimbo la Musoma Vijijini*
*www.musomavijijini.or.tz*

# WANAVIJIJI WAAMUA KUJENGA MAABARA TATU NDANI YA MIEZI MITATU

March 13, 2023



*Matukio mbalimbali ya: Harambee ya Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini ya kuchangia ujenzi wa maabara za Mtiro Sekondari. Harambee ilifanyika shuleni hapo.*

Wanavijiji wa Kata ya Bukumi wameamua kujenga Maabara 3 za Masomo ya Sayansi kwenye Sekondari yao ya Kata, Mtiro Sekondari.

Kata ya Bukumi ina vijiji vinne ambavyo ni Buira, Bukumi, Buraga na Busekera.

**Takwimu za Mtiro Sekondari**
*Ilifunguliwa Mwaka 2006
*Idadi ya wanafunzi ni 682
*Idadi ya walimu ni 17 (13 wenye ajira ya Serikali na 4 wa kujitolea)
*Hakuna Maktaba
*Hakuna Maabara hata moja ya Masomo ya Sayansi

*Wanafunzi 17 kati ya 110 wa Kidato cha Tatu (Form III), 15.5%, ndio wanasoma Masomo ya Sayansi.

*Wanafunzi 25 kati ya 123 wa Kidato cha Nne (Form IV), 20.3%, ndio wanasoma Masomo ya Sayansi.

*Wanafunzi 5 kati ya 682 ndio wamechangia chakula cha mchana.

**Harambee ya Mbunge wa Jimbo**
Alhamisi, 9.3.2023, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo aliendesha HARAMBEE shuleni hapo kwa lengo la kupata fedha za ujenzi wa Maabara 3 za Masomo ya Sayansi (Fizikia, Kemia & Baiolojia) za Mtiro Sekondari.

**Matokeo ya harambee**
*Michango ya Wanavijiji iliongozwa na Diwani wao, Mhe Munubhi Musa. Wazaliwa wa Kata ya Bukumi nao wameanza kuchangia.

**Fedha zilizochangwa:**
Tsh 494,000 (taslimu), na Tsh 4,493,000 (ahadi)
Saruji Mifuko 26
Mchanga Lori 5

*Michango ya Mbunge wa Jimbo, ameanza kwa kutoa: Saruji Mifuko 150.

**UJENZI KUANZA JUMATATU, 13.3.2023**
*Wanavijiji na Viongozi wao wa Kata ya Bukumi wameamua kuanza kutekeleza mradi huu mara moja.

*Mchanga wa kuanzia kazi tayari umesombwa

*Saruji Mifuko 75 kati ya 150 iliyotolewa na Mbunge wa Jimbo tayari imefikishwa shuleni.

*Ifikapo Juni 2023, maabara 3 ziwe zimekamilika.

**Mawasiliano ya kutoa mchango wako**

*Headmaster
Mtiro Sekondari
0758 487 478

**WADAU WA MAENDELEO:**

Wanavijiji wa Kata ya Bukumi wanaomba sana Wadau wa Maendeleo wajitokeze kuchangia utekelezaji wa mradi huu ambao ni muhimu sana kwa uboreshaji wa miundombinu ya elimu ya Mtiro Sekondari - tunatanguliza shukrani zetu za dhati kwa wachangiaji wote.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini anaendelea na kampeni yake ya kuhamasisha na kuchangia ujenzi wa Maabara 3 za Masomo ya Sayansi kwenye Sekondari zote za Jimboni mwao.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## MDAU WA MAENDELEO ACHANGIA UJENZI WA MAABARA ZA SAYANSI KWENYE SEKONDARI ZA MUSOMA VIJIJINI

March 9, 2023



*Sekondari 3 za Musoma Vijijini zikikabidhiwa Saruji Mifuko 153 kutoka Umoja Security Services yenye Makao Makuu jijini Dar es Salaam.*

Leo, Jumatano, 8.3.2023, mmoja wa Wadau wa Maendeleo hapa nchini, NGUVU MOJA SECURITY SERVICES amechangia Tsh 3,520,000 (Tsh 3.52m) kwa ajili ya ujenzi wa MAABARA ZA MASOMO YA SAYANSI (Physics, Chemistry & Biology Laboratories) kwenye baadhi ya Sekondari za Musoma Vijijini.

Mwakilishi wao, Afisa wa Polisi Mstaafu, ASP Moyo amekabidhi mchango huo kwenye Duka la kuuza vifaa vya ujenzi la Musoma Mjini. Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo, alikuwepo kushudia tukio hilo.

Jimbo la Musoma Vijijini lenye Kata 21 zenye jumla ya Vijiji 68 na Vitongoji 374 lina jumla ya Sekondari:
*25 za Kata
*2 za binafsi (Madhehebu ya Dini)

Mbunge wa Jimbo anahamasisha na kuchangia ujenzi wa Maabara za Masomo ya Sayansi kwenye Sekondari zote 27.

Lengo kuu ni kuwapatia Wanafunzi wa Sekondari zetu fursa nzuri ya kupata elimu ya vitendo, na kuongeza uelewa wao wa masomo ya sayansi.

Vile vile, ujenzi huu wa maabara tatu za masomo ya sayansi kwa kila sekondari ni matayarisho yetu ya kuanzisha HIGH SCHOOLS za MASOMO ya SAYANSI Jimboni mwetu.

**Sekondari tatu zilizopokea saruji kwa ujenzi wa maabara zao ni:**

**Seka Sekondari**
*Imepokea Saruji Mifuko 51
*Haina maabara hata moja
*Ilifunguliwa Mwaka 2021
*Mwanafunzi 344
*Walimu 7
*Hii ni Sekondari ya pili ya Kata ya Nyamrandirira

**Bwai Sekondari**
*Imepokea Saruji Mifuko 51
*Haina maabara hata moja
*Ilifunguliwa Mwaka 2023
*Mwanafunzi 139
*Walimu 5
*Hii ni Sekondari ya pili ya Kata ya Kiriba

**Muhoji Sekondari**
*Imepokea Saruji Mifuko 51
*Sekondari mpya inajengwa ifunguliwe mwakani (2024)
*Hii ni Sekondari ya pili ya Kata ya Bugwema

**TUNAKUKARIBIBISHA UCHANGIE UJENZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU KWENYE SHULE ZA MUSOMA VIJIJINI**

Usisahau kutembelea Tovuti ya Jimbo letu ambayo ni:
www.musomavijijini.or.tz

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# SEHEMU YA PILI YA TAARIFA YA KIKAO CHA MBUNGE WA JIMBO NA WAKUU WA SHULE ZA MUSOMA VIJIJINI

February 21, 2023



*Walimu Wakuu wa Sekondari za Musoma Vijijini wakiwa na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini kwenye Kikao chao cha tarehe 3.2.2023 kilichofanyika Busambara Sekondari, Kijijini Kwikuba.*

**Sehemu ya Kwanza ya Taarifa ya Kikao hicho:**

Sehemu hii ilitolewa na Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo.

*Mahali inapopatikana ni kwenye TOVUTI ya Jimbo letu ambayo ni:
www.musomavijijini.or.tz

## SEHEMU YA PILI - UFAULU WA FORM II & IV (2020, 2021& 2022)

*Kwa nini ufaulu siyo mzuri kwenye Sekondari zetu za Musoma Vijijini?

*Nini kifanyike kuongeza UELEWA na UFAULU kwa wanaojifunza (WANAFUNZI)?

*Nini kifanyike kuongeza UMAHIRI na UWAJIBIKAJI wa kufundisha kwa WALIMU wetu?

*Majukumu ya WAZAZI ni yapi?

(1) Matokeo yakutoridhisha ya Mwaka jana (2022): sababu kuu-
*Kubadilika kwa mfumo wa utungaji wa mitihani unaozingatia umahiri, yaani, "Competence Based" badala ya ule mfumo uliozoeleka wa kukariri.

Matayarisho ya mabadiliko hayo hayakuwepo.

(2) Matokeo ya kutoridhisha ya Miaka 3 mfululizo (2020, 2021 & 2022): sababu kuu -

**(2a) WANAFUNZI**

*Kutembea umbali mrefu kwenda masomoni. Wapo wanaotembea zaidi ya kilomita tano (5) kwenda masomoni

*Wanafunzi kukosa chakula wawapo masomoni (kifungua kinywa & chakula cha mchana).

*Wapo wanafunzi waliopanga vyumba kwenye vijiji vya karibu na sekondari wanazosoma. Hawa wanafunzi wapangaji wanaishi kwa kujitegemea kama ziishivyo kaya zetu.

*Sekondari nyingi hazina maabara na vifaa vyake kwa masomo ya sayansi (chemistry, physics & biology laboratories).

*Sekondari karibu zote hazina Maktaba. Vitabu vya Maktaba vipo vilivyotolewa na Mbunge wa Jimbo.

*Uhaba wa vitabu vya kiada ambapo uwiano unapaswa kuwa kitabu kimoja (1) kwa mwanafunzi mmoja (1). Uwiano huo kwa sasa, kwa baadhi ya Sekondari, ni kitabu kimoja (1) kwa wanafunzi watano (5).

*Lugha ya kufundishia ya Kiingereza bado ni tatizo.

Hata lugha yetu ya Taifa (Kiswahili) bado uelewa na ufaulu wake hauridhishi.

**(2b) Walimu**

*Upungufu mkubwa wa walimu ambao hauendani na uwiano wa walimu na wanafunzi (ratio: teacher/students). Kwa mfano ipo Sekondari ina wanafunzi 1,012 na walimu 13 tu! Ipo Sekondari mpya yenye wanafunzi 158 na walimu 5.

*Uhaba mkubwa wa walimu wa masomo ya sayansi. Kwa mfano, kuna Sekondari zenye mwalimu mmoja (1) tu wa Hisabati na mmoja (1) tu wa Fizikia kwa madarasa yote (Form I hadi IV).

*Upungufu na uhaba mkubwa wa walimu unalazimisha Sekondari kufanya yafuatayo:

(i) Kuajiri walimu wa kujitolea ambao wanalipwa posho na wazazi na Mbunge wa Jimbo huwa anachangia kwa baadhi ya Sekondari.

(ii) kuweka wanafunzi kati ya 50 na 60, au zaidi ndani ya chumba kimoja cha darasa ili kupunguza mizigo ya vipindi vyingi kwa baadhi ya walimu.

**MAPENDEKEZO YA KUONGEZA UBORA WA KUJIFUNZA NA KUFUNDISHA KWENYE SHULE ZETU**

**(1) Wanafunzi & Walimu**

*Mapungufu na mahitaji yaliyoelezwa hapo juu, kwa upande wa Wanafunzi & Walimu, yatatuliwe kwa ushirikiano wa Wahusika wote.

**(2) Wazazi**

*Wazazi watimize wajibu wao wa malezi mazuri ya watoto wao, na wafuatilie kwa karibu sana mienendo na tabia za watoto wao, k.m. kushinda kwenye luninga (TV), kubeti, kamari na kucheza pool.

*Wazazi watimize wajibu wao wa kuwanunulia watoto wao mahitaji ya shule na elimu kwa ujumla.

*Wazazi wakubali kuchangia chakula cha mchana cha watoto wao wawapo masomoni.

*Wazazi waache kuwapa watoto wao kazi za kiuchumi za familia wawapo masomoni, kwa mfano, kuwatuma kuchunga mifugo, kuvua samaki, kuchimba madini, na kuuza bidhaa sokoni wakati wa vipindi masomoni.

*Sera ya ELIMU BILA MALIPO iendelee kufanunuliwa na Wahusika ili Wazazi wasiache kutimiza wajibu wao wa kuchangia upatikanaji wa elimu nzuri kwa watoto wao.

*Wazazi na Walimu waendelee kuboresha uhusiano kati yao kwa manufaa ya uboreshaji wa elimu itolewayo kwenye shule zao.

**(3) Walimu**

*Walimu waongezewe mafunzo wawapo kazini. Mafunzo yatolewe mara kwa mara ndani ya kipindi kifupi cha miaka 2-3.

*Kuwepo msawazo sawa kwa wingi (fair distribution) wa walimu kwenye Sekondari za vijijini na mijini ndani ya Halmashauri, Wilaya na Mkoa.

*Maslahi ya walimu yaboreshwe kwa kiwango kikubwa, yaani:

(i) Walimu wajengewe nyumba za kuishi hasa wale wanaofundisha vijijini.

(ii) Mishahara ya Walimu iboreshwe sana na makato yake yapunguzwe.

Nchi ambazo zinaongoza Dunia kwa ubora wa elimu, mishahara ya walimu wao iko juu kuzidi taaluma nyingi nchini humo.

*Kitengo cha uthibiti ubora kiongezewe uwezo wa kufuatilia shughuli za ufundishaji na ujifunzaji mashuleni.

*Kuimarisha lugha za kufundishia na kujifunzia kwa shule za Msingi na Sekondari.

*Kutoa motisha kwa wanafunzi na walimu wanaofanya vizuri kwenye mitihani inayotolewa.

*Waliopewa majukumu ya kiuongozi ya kusimamia masuala ya elimu kwenye mashule wawe na uwezo wa kielimu wa kutekeleza majukumu yao.

## SEKA SEKONDARI – WANAVIJIJI WAAMUA KUJENGA MAABARA TATU ZA MASOMO YA SAYANSI

February 5, 2023



*Seka Sekondari ni sekondari ya pili ya Kata ya Nyamrandirira yenye vijiji vitano.*

Sekondari hii iliyojengwa Kijijini Seka, Musoma Vijijini, ilifunguliwa tarehe 5.7.2021.

Sekondari ina jumla ya wanafunzi 344 (Vidato vya I, II & III) na Walimu tisa (9), mmoja akiwa ni wa kujitolea.

**Mapungufu makubwa na muhimu ni ukosefu wa:**
*Maabara 3 za masomo ya sayansi ya Fizikia, Kemia na Baiolojia.
*Maktaba
*Choo kingine chenye matundu 7
*Jengo la Utawala

## HARAMBEE YA MBUNGE WA JIMBO

Leo, Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo, ameendesha HARAMBEE shuleni hapo kwa ajili ujenzi wa MAABARA 3 za masomo ya Sayansi.

**Matokeo ya harambee ya leo:**

*Wanavijiji wameamua kwamba Maabara hizo zikamilike ifikapo tarehe 30 Juni 2023.

*Wanavijiji watachangia nguvukazi na Tsh 15,000 kila Kaya.

*Vifaa vya ujenzi vilivyosalia kwenye ujenzi wa kutumia fedha za Serikali, vitumike mara moja, ikiwemo Saruji Mifuko 60.

*Viongozi mbalimbali wa Kata hiyo, wakiongozwa na Diwani wao, Mhe Mwl Nyeoje wamechangia Saruji Mifuko 12 na fedha taslimu Tsh 100,000.

**Michango ya Mbunge wa Jimbo:**
*Saruji Mifuko 150
*Vitabu vya Maktaba box saba (7)
*Mahindi magunia manne (4) ya chakula cha wanafunzi

**OMBI MAALUM LA UONGOZI WA SHULE:**
Seka Sekondari isaidiwe kupata, computer, printer na photocopying machine - Wanakijiji na Mbunge wao wa Jimbo, watachanga kwa pamoja na kuvinunua ifikapo 30.4.2023.

## MICHANGO YA AWALI YA UJENZI WA SEKA SEKONDARI

Sekondari hii ilianza kujengwa kwa nguvu za WANAVIJIJI, MBUNGE WA JIMBO, WAZALIWA WA KATA YA NYAMRANDIRIRA na baadae SERIKALI imetoa michango mikubwa.

## MICHANGO HIYO NI KAMA IFUATAVYO:

**Wanavijiji**

*Nguvukazi - kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji

*Kijiji cha Seka kilijenga na kuezeka vyumba 3 vya madarasa na kununua samani za ofisi za walimu.

*Kijiji cha Kasoma kilijenga na kuezeka vyumba 2 vya madarasa.

*Vijiji vya Mikuyu & Kaboni vilijenga na kuezeka maboma 2 ya madarasa.

*Kijiji cha Chumwi kilichangia ujenzi wa boma moja la darasa na ujenzi wa choo cha walimu.

*Wazazi wanachangia malipo ya posho za walimu wa kujitolea.

SERIKALI imechangia, kwa nyakati tofauti, Tsh MILIONI 25 + 80 + 60. Vifaa vya Maabara na Tsh 891,436, - kila mwezi (uendeshaji) kuanzia Oktoba 2022.

Wanavijiji wa Kata ya Nyamrandirira na Viongozi wao mbalimbali wanatoa shukrani za kipekee kwa Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa mchango mkubwa unaotolewa na Serikali kwa ujenzi wa Sekondari yao - AHSANTE SANA.

**Mbunge wa Jimbo**
Michango yake ya awali, kwa nyakati tofauti, ni:
*Saruji Mifuko 200
*Mabati 120

**Mfuko wa Jimbo umechangia:**
*Saruji Mifuko 330
*Mabati 137
*Nondo 17

**Wazaliwa wa Kata ya Nyamrandirira**
Wazaliwa wa Kata hii wamechangia jumla ya Tsh 2,840,000.

HALMASHAURI yetu hadi sasa mchango wake ni Saruji Mifuko 30 tu.

**Mgodi wa Seka**
Mchango wa Mgodi huu (MMG) wa dhahabu ni mdogo na hauridhishi.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## HARAMBEE ZA MBUNGE WA JIMBO: SARUJI INAENDELEA KUTOLEWA

February 2, 2023



*Viongozi kutoka Muhoji Sekondari wakipokea Saruji Mifuko 50*

Jumatano, 25.1.2023, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo alitoa SARUJI MIFUKO 50 kuchangia ujenzi wa Sekondari mpya ya Kijijini Muhoji, Kata ya Bugwema.

Hiyo ni sehemu ya SARUJI MIFUKO 150 aliyoahidi kwenye HARAMBEE ya jana ya kuchangia Muhoji Sekondari.

Viongozi kutoka Muhoji Sekondari walikuwepo kupokea Saruji Mifuko 50.

Hii ni Sekondari ya pili ya Kata ya Bugwema.

Pia, Mbunge huyo aliipatia Bwai Sekondari SARUJI MIFUKO 50 na MABATI BUNDLE 2 (mabati 24) Hii ni matokeo ya HARAMBEE ya tarehe 19.1.2023.

Bwai Sekondari ikimaliza hiyo mifuko 50, itapewa mifuko mingine 50. Ahadi ya Mbunge huyo ni kuchangia jumla ya saruji mifuko 100.

Hii ni Sekondari ya pili ya Kata ya Kiriba.

**KARIBUNI TUCHANGIE KWA VITENDO UJENZI NA UBORESHAJI WA SHULE ZETU**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# HARAMBEE YA UJENZI WA SEKONDARI MPYA KIJIJINI MUHOJI

January 25, 2023



*Harambee ya ujenzi wa Muhoji Sekondari ya Kijijini Muhoji, Kata ya Bugwema.*

Kijiji cha Muhoji ni moja kati ya vijiji vinne (4) vya Kata ya Bugwema - vingine ni Masinono, Kinyang'erere na Bugwema.

**Kata hii ina Sekondari moja iitwayo Bugwema ambayo kwa sasa imeelemewa sana kwa sababu zifuatazo:-**

*Kidato cha Kwanza (Form I) cha mwaka huu (2023) kina jumla ya WANAFUNZI 362 walioko kwenye Mikondo 7 ya wanafunzi 50 kwa kila mkondo. Iwapo kila mkondo ungalikuwa wa Wanafunzi 40, Form I hii ingalikuwa na Mikondo 9.

*Walimu 10 tu kwa Sekondari yenye jumla ya Wanafunzi 748.

Mbali ya mirundikano hiyo kwenye Bugwema Sekondari, bado wanafunzi wa kutoka Kijiji cha Muhoji wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 24-30 kwenda na kurudu kutoka masomoni.

**HARAMBEE YA MBUNGE WA JIMBO**

Leo, Jumanne, 24.1.2023, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo ameendesha HARAMBEE ya kuchangia ujenzi wa MUHOJI SEKONDARI.

**Michango iliyopatikana**

(i) Wanakijijiji wakiongozwa na Diwani wa Kata, Mhe Clifford Machumu wamechangia:
*Saruji Mifuko 124.
*Fedha taslimu, Tsh 305,000.

**Michango hiyo ya wananchi ni mbali na michango yao mingine ya:**
*Nguvukazi - kusomba mawe, mchanga na kokoto.
*Tsh 45,000 kwa kila kaya

(ii) DC wa Wilaya ya Musoma, Mhe Dkt Halfan Haule amechangia:
*Saruji Mifuko 20.
*Jana alishiriki kwenye ufyatuaji wa matofali.

(iii) Mbunge wa Jimbo amechangia:
*Saruji Mifuko 150
*Ataendelea kuchangia.

**MALENGO YALIYOWEKWA;**

*Ujenzi wa Vyumba 4 vya Madarasa vyenye Ofisi 2 (katikati) za Walimu na Choo chenye Matundu 8 ukamilike kabla ya 30 Julai 2023.

*Muhoji Sekondari ifunguliwe Januari 2024

TUNAKARIBISHWA kuchangia ujenzi wa Muhoji Sekondari. Mchango wako mpelekee:
Mtendaji wa Kijiji (VEO)
Samwel Mourice
0686 557 264
0769 458 012

**ELIMU NI UCHUMI**
**ELIMU NI MAENDELEO**
**KARIBU TUCHANGIE UJENZI WA SHULE ZETU**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI

# WA

# MIRADI

# YA

# AFYA

# (30 Juni 2023 – 1 Julai 2022)

## KATA YA BUKUMI INAYOJENGA ZAHANATI 3 NA VYUMBA VIPYA VYA MADARASA YAPEWA SARUJI MIFUKO 200

August 4, 2022



*Wasaidizi wa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini wakikabidhi SARUJI MIFUKO 200 kwa Viongozi wa Kata ya Bukumi. Hii ilitokea leo, Jumatano, 3.8.2022, Musoma Mjini.*

Jumatano, 3.8.2022, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini ametoa SARUJI MIFUKO 200 (mia mbili) kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa Zahanati 3 na Vyumba vipya 2 vya Madarasa ndani ya Kata ya Bukumi.

Kata ya Bukumi yenye vijiji vinne (Buira, Bukumi, Buraga na Busekera) ina Zahanati moja tu, ambayo iko kwenye Kijiji cha Buraga, Kitongoji cha Kurugee.

Vijiji vingine vitatu vimeamua kujenga Zahanati zake na ujenzi tayari umeanza kwa kasi ya kuridhisha.

**MICHANGO YA WANAVIJIJI NI:**

*Nguvukazi
*Fedha taslimu, Tsh 10,000 – 15,000

DIWANI wa Kata, Mhe Munubhi Musa amechangia Tsh 100,000 (laki moja) kwa kila Zahanati. Jumla Tsh 300,000 (laki tatu).

MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo amechangia SARUJI MIFUKO 50 kwa kila Zahanati na MIFUKO mingine 50 kwa ajili ya ujenzi wa Vyumba vipya 2 vya Madarasa ya S/M Busekera.

Kwa hiyo, Mbunge huyo amechanga jumla ya SARUJI MIFUKO 200 yenye thamani ya Tsh 4.5 million.

MICHANGO mingine ya Mbunge huyo kwenye Sekta ya Afya ndani ya Kata hiyo ni kama ifuatavyo:

*Gari la Wagonjwa (Ambulance) kwa Zahanati ya Kurugee, Kijijini Buraga

*Saruji Mifuko 100 (mia moja) kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Bukumi inayojengwa kwenye Kitongoji cha Kukema Burungu.

**HUDUMA ZA AFYA NDANI YA JIMBO LETU:**
Jimbo letu lina Kata 21 zenye jumla ya Vijiji 68. Huduma za Afya zinatolewa na:

*Hospitali ya Wilaya ambayo bado inaendelea kujengwa
*Vituo vya Afya: 3

*Zahanati za Serikali: 23
*Zahanati Binafsi: 4

**UJENZI UNAOENDELEA:**
*Vituo vya Afya: 3
*Zahanati za Vijiji zinazojengwa: 17

**OMBI KUTOKA KATA YA BUKUMI**

Wana-Kata ya Bukumi na rafiki zetu tunaombwa tujitokeze kuchangia miradi hii ya ujenzi iliyoanzishwa na inatekelezwa kwa nguvukazi na michango ya fedha taslimu kutoka kwa wanavijiji wenyewe.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# SERIKALI YAENDELEA KUSHIRIKIANA NA WANAVIJIJI KWENYE UJENZI WA VITUO VIPYA VYA AFYA VYA MUSOMA VIJIJINI

June 14, 2022



*Ujenzi unaoendelea wa Kituo kipya cha Afya cha Kata ya Makojo kinachojengwa Kijijini Makojo.*

Jimbo la Musoma Vijijini lenye Kata 21 zenye jumla ya Vijiji 68, lina Kata 3 zenye Vituo vya Afya vinavyofanya kazi. Vituo hivyo ni vya:

*Murangi
*Mugango
*Bugwema

Serikali inaendelea kutoa fedha kwenye ujenzi wa Vituo vipya vya Afya, ambavyo ni:
*Kisiwa cha Rukuba
*Makojo
*Kiriba

Kwenye ujenzi huo, Serikali ilitoa Tsh milioni 250 (Tsh 250m) kwa kila Kituo kuanza ujenzi wake.

Serikali imetoa tena Tsh milioni 250 (Tsh 250m) kuendeleza ujenzi wa Vituo hivyo vipya. Fedha hizo za awamu ya pili zitapelekwa kwenye Kata husika siku chache zijazo.

Mchango wa Tsh milioni 500 (Tsh 500m) kwa kila Kituo kipya kinachojengwa Jimboni mwetu ni mchango mkubwa. Tunaishukuru sana Serikali yetu na kipikee kabisa tunamshukuru sana Rais wetu, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha fedha za utekelezaji wa miradi hii na mingine zinapatakina – Ahsante sana!

**Jumla ya ZAHANATI zinazotoa huduma za Afya Jimboni mwetu ni:**

*22 za Serikali
*4 za Binafsi

**Jumla ya ZAHANATI mpya zinazojengwa ni**:

*15 zinajengwa na WANAVIJIJI na baadhi zimepokea michango ya fedha kutoka Serikalini.

MICHANGO ya NGUVUKAZI za WANAVIJIJI inaombwa iendelee kutolewa hadi kukamilika kwa ujenzi wa VITUO VIPYA VYA AFYA na ZAHANATI zinazojengwa.

Usisahau kutembelea TOVUTI ya Jimbo letu ambayo ni:
www.musomavijijini.or.tz

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KILIMO, UVUVI NA UFUGAJI

# (30 Juni 2023 – 1 Julai 2022)

# SERIKALI YARIDHIA KUFUFUA MRADI MKUBWA WA KILIMO CHA UMWAGILIAJI NDANI YA BONDE LA BUGWEMA

January 3, 2023



*Timu ya Wataalamu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji wakiwa ndani ya Bonde la Bugwema, Musoma Vijijini. Baadhi ya Viongozi wa Musoma Vijijini walishiriki kwenye ziara hiyo.*

*Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikusudia kuanzisha kilimo kikubwa cha umwagiliaji ndani ya Bonde la Bugwema. Hii ilikuwa mwanzoni mwa miaka ya 70.

*Bonde la Bugwena ni kubwa mno. Eneo lililokusudiwa kulimwa wakati huo ilikuwa ni ndani ya Hekta 10,000. Bonde lenyewe likichukuliwa kwa ujumla wake lina ukubwa wa zaidi ya Hekta 20,000.

*Miundombinu ya umwagiliaji ilijengwa miaka hiyo, lakini utekelezaji wake ukasimama.

*Mazao makuu yanayolimwa ndani ya Bonde hilo ni mahindi, mpunga, alizeti, dengu na pamba.

*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan ameridhia ombi la kuendeleza Mradi huo wa Bugwema.

*Ombi hilo lilitolewa na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo wakati Mhe Rais wetu alipotembelea Musoma Vijijini akizindua Mradi wa ujenzi wa Bomba la Maji la Mugango-Kiabakari-Butiama. Hii ilikuwa tarehe 6 Februari 2022.

*Mbunge huyo alirudia kutoa ombi hilo kwenye Mkutano Mkuu wa CCM uliofanyika Dodoma, tarehe 7-8.12.2022.

*Jana, Alhamisi, 29.12.2022, Timu ya Wataalamu kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilitembelea Bonde la Bugwema. Timu hiyo iliongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Dr Raymond Mndolwa.

**Viongozi kadhaa wa Musoma Vijijini waliambatana na Timu hiyo ya Wataalamu. Baadhi yao ni:**
*Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo.
*Mwenyekiti wa CCM wa Kata ya Bugwema, Ndugu Ezekiel MacGudo.
*Diwani wa Kata ya Bugwema, Mhe Clifford Machumu.
*Mtendaji wa Kata ya Bugwema, Ndugu Joseph Phinias.

Taarifa iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ni kwamba matayarisho ya utekelezaji wa Mradi wa Bugwema yanaendelea vizuri kwa ajili ya kuanza kufanya "feasibility studies and designs."

Musoma Vijijini wanaendelea kutoa shukrani nyingi sana kwa Rais wetu, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kuendeleza Mradi wa Kilimo kikubwa cha Umwagiliaji ndani ya Bonde la Bugwema.

Upatikanaji wa chakula kingi cha bei nafuu kunasaidia kushusha mfumuko wa bei kwenye soko la chakula.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## MVUA ZA VULI – MICHE LAKI MOJA (100,000) YA MITI NA MATUNDA KUSAMBAZWA NA KUPANDWA MUSOMA VIJIJINI

October 27, 2022



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo akiwa kwenye Kitalu cha VI Agroforest kinachotayarisha miche laki moja (100,000) ya miti na matunda.*

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo anaendelea kushirikiana na VI Agroforest kugawa bure miche ya miti na matunda kwa wanavijijini na taasisi mbalimbali (k.m. shule, zahanati) Jimboni mwao.

VI Agroforest inafadhiliwa na Serikali ya Sweden na inafanya kazi nzuri ya utunzaji wa mazingira ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini na kwingineko Mkoani Mara.

Miche laki moja (100,000) itakayogawiwa bure wakati wa mvua za vuli (Novemba-Disemba 2022) itakuwa ya miti ya:

*Matunda
*Mbao/ujenzi
*Kuni
*Ufugaji wa nyuki
*Madawa ya asili

Matayarisho ya miche laki moja (100,000), chini ya Mtaalamu Jacob Malima, yanaendelea vizuri ndani ya Kitalu cha VI Agroforest kilichopo Mjini Musoma.

**OMBI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**
Jimbo la Musoma Vijijini linaiomba Wizara hiyo ifufue Kitalu cha Miti cha Serikali kilichopo Kijijini Suguti.

Usisahau kutembelea TOVUTI ya Jimbo letu ambayo ni: www.musomavijijini.or.tz

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WAKULIMA MASHUHURI WA ALIZETI WAJENGA KIWANDA KIDOGO CHA KUSINDIKA MBEGU ZA ALIZETI

September 11, 2022



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo akiwa ndani ya kiwanda kidogo cha kusindika mbegu za alizeti. Kiwanda hicho kitakachofunguliwa mwezi huu kinajengwa Kijijini Masinono, Kata ya Bugwema.*

Ijumaa, 9.9.2022, Kikundi cha Changamkeni cha Kijijini Masinono, Kata ya Bugwema kimekamilisha malipo ya kufungiwa umeme kwenye KIWANDA chao cha ALIZETI kinachojengwa Kijijini Masinono. Mbunge wa Jimbo nae amechangia gharama za kufungiwa umeme kwenye kiwanda hicho.

**UNUNUZI WA MASHINE YA KUKAMUA MBEGU ZA ALIZETI**

*Mwaka 2020, Shirika la SHIMAKIUMU linalojishughulisha na Kilimo na Ufugaji ndani ya Wilaya yetu, lilipatia Kikundi cha Changamkeni mashine ya kukamua mbegu za alizeti.

*Mashine hiyo ina thamani ya Tsh Milioni 35 (Tshs 35m) na uwezo wa kukamua mbegu za alizeti kwa kiasi cha magunia 40 kwa siku.

Shukrani za dhati zinatolewa kwa SHIMAKIUMU kwa ufadhili huo utakaofaidisha Wana Kikundi cha Changamkeni, na wakulima wengine wa alizeti ndani ya Bonde la Bugwema na kwingineko Mkoani Mara.

**KILIMO CHA ALIZETI MUSOMA VIJIJINI**

Mbunge Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo alianza kampeni ya kushawishi uanzishwaji wa kilimo cha alizeti Jimboni mwao Mwaka 2016, na kwa misimu mitatu mfululizo (ya kilimo) aligawa bure mbegu za alizeti kiasi cha TANI 9.66. Msimu wa Mwaka 2018/2019, Wizara ya Kilimo ilichangia TANI 10.

**BUGWEMA YAONGOZA KWENYE KILIMO CHA ALIZETI**

Wakulima ndani ya Bonde la Bugwema ndio wanaongoza kwa kilimo cha zao la alizeti ndani ya Mkoa wa Mara.

Kikundi cha Changamkeni kinakusudia kulima Ekari 500 za alizeti ndani ya Bonde la Bugwema.

Mazao mengine yanayolimwa kwa wingi na wakulima wa ndani ya Bonde la Bugwema ni: mahindi, mpunga, dengu na pamba.

Wakulima wa Bugwema wanasubiri kwa hamu kubwa Mradi kabambe wa umwagiliaji ndani ya Bonde la Bugwema. Mradi huo utaanza kwa ufadhili ya Serikali yetu.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI

# WA

# MIRADI

# YA

# MAJI

# (30 Juni 2023 – 1 Julai 2022)

## WANAVIJIJI WAPATA MATUMAINI MAKUBWA YA KUANZA KUTUMIA MAJI YA BOMBA

June 16, 2023



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijinini, Prof Sospeter Muhongo akiongea na WANANCHI wa Vijiji 3 (Tegeruka, Mayani na Kataryo) vya Kata ya Tegeruka. Hiyo ilikuwa siku ya Jumapili, 11.6.2023 wakati Mbunge huyo alipofanya ukaguzi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji ya bomba kwenye vijiji hivyo.*

Kata nne (4) zenye jumla ya Vijiji 12, za Jimbo la Musoma Vijijini, zina miradi ya kusambaziwa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria.

Mradi wa Bomba Kuu la Maji la Mugango-Kiabakari-Butiama
*Gharama za Mradi: Tsh bilioni 70.5.
*Uwezo wa uzalishaji: Lita milioni 35 kwa siku.
*Mitambo ya kusukuma maji inayotengenezwa China, Hungary na Turkey italetwa nchini hivi karibuni.

Ujenzi wa Miundombinu ya usambazaji wa maji ya bomba kutoka Bomba Kuu la Mugango-Kiabakari-Butiama

**Kata za Tegeruka na Mugango**
*Gharama za Mradi: Tsh bilioni 4.75
*Ujenzi umeanza tokea wiki iliyopita na Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo alienda kukagua ujenzi huo.
*Mitaro ya urefu wa takriban km 15 tayari imechimbwa na bomba zitaanza kutandazwa hivi karibuni
*Tenki lenye ujazo wa LITA 135,000 linajengwa Kijijini Mayani. Hili tenki litapokea maji kutoka kwenye Tenki la Kijijini Kiabakari lenye ujazo wa LITA MILIONI 3

**Kata za Busambara na Kiriba**
*Tenki la ujazo wa LITA 500,000 limejengwa kwenye Mlima Kong'u, Kijijini Kwibara, Kata ya Mugango.

*Vijiji 6 vya Kata za Busambara na Kiriba vitapata maji ya bomba kutoka kwenye Tenki hili.

*Miundombinu ya usambazaji wa maji ya bomba kwenye Kata hizi mbili itaanza kujengwa, hivi karibuni, August 2023.

**SHUKRANI:**
Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanaishukuru sana Serikali yetu chini ya uongozi mzuri wa Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji ya bomba vijijini mwetu. Kila kijiji kinao mradi wa maji - Ahsante sana!

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MRADI WA BOMBA LA MAJI LA MUGANGO-KIABAKARI-BUTIAMA WAKAGULIWA NA KAMATI YA BUNGE

January 16, 2023




*Mh. Mbunge wa Musoma Vijijini Prof Sospeter Muhongo akitoa mchango wake wakati wa ukaguzi huo.*

Jumamosi, 14.1.2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikagua Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Bomba la Maji la Mugango-Kiabakari- Butiama.

**Gharama ya Mradi huu ni kubwa:**

Tsh bilioni 70.5 kutoka Serikali ya Saudi Arabia (49.12%), BADEA (31.40%) na Serikali ya Tanzania (19.48%)

Tsh bilioni 4.775 za Serikali ya Tanzania kwa ajili kujenga miundombinu ya usambazaji wa maji kwenye Kata za Mugango na Tegeruka.

Choteo la maji lilojengwa Kijijini Kwibara, Kata ya Mugango, Musoma Vijijini, lina uwezo wa kuchota LITA MILIONI 35 KWA SIKU.

Kamati ya Bunge imerdhishwa na utekelezaji wa Mradi huu ambao utakamilika ifikapo tarehe 30 Juni 2023.

Usisahau kutembelea TOVUTI ya Jimbo letu ambayo ni: www.musomavijijini.or.tz

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## ZAIDI YA BILIONI 4 KUSAMBAZA MAJI KATA ZA TEGERUKA NA MUGANGO

January 7, 2023



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga ameelekeza ifikapo Februari, 2023 utekelezaji wa mradi wa kufikisha maji kwenye Kata za Mugango na Tegeruka za Musoma Vijijini uwe umeanza ili ifikapo Mwezi Juni, 2023 wananchi wawe wanapata maji.

Katibu Mkuu huyo ametoa maelekezo kwa nyakati tofauti Januari 5, 2023 mbele ya Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo kwenye mikutano ya hadhara na wananchi wa Kata hizo, maelekezo hayo yametolewa kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji Mkoani Mara ambazo ni Mamlaka ya Maji Musoma (MUWASA), Mamlaka ya Maji Mugango-Kiabakari-Butiama na RUWASA Mkoa wa Mara.

Katibu Mkuu huyo amesema utekelezwaji wa mradi huo ni maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa bomba la maji la Mugango-Kiabakari-Butiama tarehe 6 Februari, 2022.

“Mtakumbuka Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dokta Samia Suluhu Hassan alifika hapa na kutuwekea jiwe la msingi la mradi wenye thamani ya shilingi bilioni 70.5. Katika mradi huo palikuwa na awamu mbili za utekelezaji lakini maelekezo yake yalikuwa ni kwamba mradi uwe na awamu moja badala ya kuwa na awamu mbili,” amesema Mhandisi Sanga.

Katibu Mkuu huyo amebainisha kuwa ziara yake wilayani humo imelenga kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa Mugango-Kiabakari-Butiama lakini pia kutoa maelekezo mbalimbali kuhusiana na maendeleo ya utekelezaji sambamba na kuzungumza na wananchi wa Kata za Mugango na Tegaruka ili kuwafahamisha kuhusiana na neema inayokuja ya kufikishiwa huduma ya maji.

“Nimefika hapa kuzungumza na wananchi wa vijiji vyote vya Kata za Mugango na Tegeruka kuwafahamisha kuwa Mheshimiwa Rais Dokta Samia Suluhu Hassan ametuongezea shilingi bilioni 4.775 kwa ajili ya kuhakikisha mnapata huduma ya maji kupitia mradi huu mkubwa wa Mugango-Kiabakari-Butiama,” anabainisha Mhandisi Sanga.

Mhandisi Sanga ameelekeza wataalam watakaosimamia utekelezaji wa mradi huo kuhakikisha ndani ya mwezi huu wa Januari, 2023 watafute wakandarasi wengine tofauti na huyo anayetekeleza mradi mkubwa ili ikifika mwezi Februari wasaini mikataba na kuanza utekelezaji lengo likiwa ni kwamba pindi mradi mkubwa unavyokamilika mwezi Juni, 2023 wananchi wote wanapata huduma.

Mhandisi Sanga amewaasa wananchi wa kata hizo kuepuka kusikiliza maneno ya mitaani yanayotolewa na wasiopenda maendeleo ya kwamba hawatopata maji. “Kumekuwa na wapotoshaji ambao wanakuelezeni kwamba mnadanganywa, niwahakikishie ndugu zangu Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dokta Samia Suluhu Hassan imejipambanua vyema katika kukabiliana na kero zinazowatatiza wananchi wake,” amebainisha Mhandisi Sanga.

Aidha, Katibu Mkuu huyo alimpongeza Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara wa miradi ya maji na aliwaomba radhi wananchi wa Kata hizo kwa kuchelewa kuanza utekelezaji kwa kuwa walikuwa wakisubiri ujenzi wa mradi mkubwa usogee ambao ndio chanzo cha maji cha mradi husika ili yote ikamilike kwa pamoja.

“Tulichelewa kuanza utekelezaji kwa kuwa utatoa maji kwenye mradi mkubwa sasa endapo tungelaza tu mabomba yangelikuwa hayana maji lakini kwa sasa ni wakati muafaka tuanze ili mradi mkubwa unapokamilika hapo Juni na hapa tunakuwa tumekamilisha,” anafafanua Mhandisi Sanga.

Akizungumzia mradi wa Mugango-Kiabakari-Butiama, Mhandisi Sanga amesema maelekezo yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Meja Jenerali Suleiman Mzee alipofanya ziara kwenye mradi Desemba, 2022 ndiyo maelekezo ya Wizara ya Maji.

“Mtakumbuka hivi karibuni Mkuu wa Mkoa alitembelea hapa na alitoa maelekeozo kwa wakandarasi na wasimamizi kwamba ifikapo tarehe 30 Juni, 2023 mradi uwe umekamilika na hakuna muda wa nyongeza nasi tunaungana na maelekezo yake na tunasisitiza aliyoyaelekeza yabaki vilevile ifikapo tarehe 30 mradi uwe umekamilika,” amesisitiza Mhandisi Sanga.

Kwa upande wake, Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo amesema ameshuhudia jitihada za Serikali kupitia Wizara ya Maji za kumtua mama ndoo ya maji kichwani ambapo amebainisha kuwa vijiji vingi vilivyoko pembezoni mwa Ziwa Victoria tayari vina huduma ya maji.

Mbunge huyo amebainisha kuwa baadhi ya Kata za Jimboni mwake zikiwemo Kata ya Etaro, Nyegina, Ifulifu, Nyakatende watatumia maji kutoka Musoma mjini na jukumu hilo tayari Wizara ya Maji imelitolea maelekezo kwa MUWASA ya kuhakikisha vinafikishiwa huduma.

"Ninaendelea kuwathibitishia namna ambavyo Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan inavyopenda Jimbo la Musoma Vijijini, mwaka huu tunaouanza Serikali inazidi kuwekeza fedha nyingi ndani ya Jimbo letu. Mbali na mradi wa Mugango – Kiabakari - Butiama tumeletewa miradi mingine," amesema Profesa Muhongo.

Mbunge huyo amebainisha kuwa kwa Kata ya Mugango tayari kuna miradi miwili mmoja ikiwa ni huo aliyouzungumzia Mhandisi Sanga na kwamba kabla ya mradi huo Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliwapatia fedha kiasi cha Shilingi Milioni 600 ambazo walizigawana na Butiama, na kwamba fedha hizo zimewezesha maeneo mengi kupata huduma ya maji maeneo ya Kaburabura, Bugoji, Kanderema, Saragana, Nyambono na Mikuyu kufikishiwa huduma ya maji.

Imetolewa na Mwandishi wa Habari
Wizara ya Maji
5.1.2023

# MRADI WA MAJI WA CHITARE - MAKOJO UMEANZA KUKAMILIKA

December 2, 2022




*RUWASA inaendelea kujenga miundombinu yenye ubora na sasa WANAKIJIJI wa CHITARE wameanza kupata maji safi na salama ya bomba.*

Vijiji vya Chitare na Makojo vya Kata ya Makojo vimesubiri maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria tokea Mwaka 2013.

Mradi huu ulioanzwa kutekelezwa na Halmashauri yetu (Musoma DC) tokea Mwaka wa Fedha 2013/2014, sasa unarudiwa na unakamilishwa kwa ubora mzuri na RUWASA.

RUWASA inaendelea kujenga miundombinu yenye ubora na sasa WANAKIJIJI wa CHITARE wameanza kupata maji safi na salama ya bomba.

Kwa muda mfupi ujao, Wanakijiji wa Makojo nao watapata maji ya bomba hilo.

Tumeomba bomba hilo lijengwe hadi Kijiji cha Chimati ambacho nacho kiko ndani ya Kata ya Makojo. Serikali imepokea ombi letu na kukubali kulitekeleza.

RUWASA inaendelea kufanya kazi zenye ubora mzuri ndani ya Jimbo letu.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI

# WA

# MIRADI

# YA

# UJENZI WA BARABARA

# (30 Juni 2023 – 1 Julai 2022)

## BARABARA KUU PEKEE YA MUSOMA VIJIJINI INAHITAJI KUWEKEWA LAMI: HAIJAPITIKA KIURAHISI KWA ZAIDI SIKU TANO (5)

April 3, 2023



*Eneo la maafa, Kijiji cha Kusenyi, Kitongoji cha Kwikuyu, Musoma Vijijini.*

**Barabara ya Musoma-Makojo-Busekera (km 92)**

*Mvua zinazonyeesha wakati huu zinaleta maafa kwa baadhi ya vijiji vilivyoko pembezoni mwa barabara hii.

*Jana usiku na leo asubuhi, Kijiji cha Kusenyi, Kitongoji cha Kwikuyu kimekumbwa na mafuriko makubwa. Wakazi wa hapo wamepoteza mali zao, kikiwemo chakula walichokuwa wamehifadhi majumbani mwao.

*Mkandarasi aliyejenga km 5 kwenye hili barabara la urefu wa km 92 analalamikiwa kwa kuziba vidaraja vidogo vidogo vilivyokuwa vinapitisha maji kwenda ziwani (Ziwa Victoria)

**Umuhimu wa barabara ya Musoma-Makojo-Busekera.**

*Vijiji 68 vya Musoma Vijijini vinaunganishwa na barabara kuu moja tu, ambayo ni hii ya Musoma-Makojo-Busekera.

*Barabara hii inaunganisha Musoma Vijijini na Wilaya nyingine za Mkoa wa Mara, na hatimae inaunganisha Musoma Vijijini na Mikoa ya jirani ya Mwanza, Simiyu, Manyara na Arusha

*Barabara hii inaunganisha Musoma Vijijini na Kiwanja cha Ndege cha Musoma Mjini (& Mwanza), na Bandari ya Meli iliyopo Musoma Mjini

*Mazao ya uvuvi (dagaa, sangara na sato) yanasafirishwa kutumia barabara hii.

*Mazao ya Kilimo, yaani, mihogo, viazi vitamu, mpunga, mahindi, mtama, matunda, mbogamboga, pamba, alizeti, n.k. yanasafirishwa kutumia barabara hii.

*Dhahabu na madini mengine yanasafirishwa kutumia barabara hii.

**Wizara ya Ujenzi & Uchukuzi**

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo na Viongozi wengine wa Chama (CCM) na Serikali wanaendelea kuiomba Wizara ya Ujenzi & Uchukuzi kuipa kipaumbele barabara hili ijengwe kwa kiwango cha lami.

Maombi ya Wana Musoma Vijijini na Viongozi wao ya barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami ni tokea Mwaka 1980.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## HATIMAYE MUSOMA VIJIJINI WAANZA KUPATA BARABARA YA LAMI

September 15, 2022



*Mradi wa ujenzi wa barabara ya lami ya Musoma-Makojo-Busekera (km 92) unaanza kuweka matumaini.*

**KILOMITA 5 KUKAMILIKA OKTOBA 2022**

Kampuni ya Gemen Engineering inayojenga kilomita hizo tano (5) imesema itakamilisha na kukabidhi kipande hicho cha kilomita 5 ifikapo tarehe 30.10.2022. Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa kampuni hiyo Injinia Andrew Nyantori.

Leo, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo alikagua ujenzi wa barabara hilo ili ajiridhishe na ahadi ya Mkandarasi huyo.

**UMUHIMU WA BARABARA HILI KIUCHUMI**

Barabara hili ndiyo roho ya ukuaji wa uchumi wa Jimbo la Musoma Vijijini lenye Kata 21, Vijiji 68 na Vitongoji 374.

Samaki wengi na wa aina mbalimbali wanaovuliwa Ziwa Victoria wanasafirishwa kutoka Musoma Vijijini kwenda kwenye masoko mbalimbali ya ndani na ya nje ya nchi yetu kwa kutumia barabara hili.

Mazao ya chakula ambayo nayo ni ya biashara (k.m. mihogo, mahindi, viazi vitamu, mpunga, na matunda) yanasafirishwa kutumia barabara hili.

Musoma Vijijini ni maarufu kwa kilimo cha pamba. Barabara hili ndilo linatumika kusafirisha pamba kutoka vijijini mwetu kwenda sokoni.

Dhahabu na madini mengine yanayochimbwa Musoma Vijijini yanasafirishwa kwa kutumia barabara hili.

**UMUHIMU WA BARABARA HILI KWA HUDUMA ZA JAMII**

*Hili ndilo barabara kuu na pekee linalounganisha vijiji vyote 68 vya Jimboni mwetu. Kwa hiyo, hili barabara ni muhimu sana kwa usafiri wa wananchi ndani na nje ya Jimbo letu.

*Hili ndilo barabara kuu na pekee ambalo linatumika kwa usambazaji wa vifaa vya elimu, huduma za afya, kilimo, ufugaji, maji, umeme, n.k., ndani ya Jimbo letu.

*Wagonjwa wanaohitaji matibabu kwenye hospital kubwa za Musoma, Mwanza, n.k. wanatumia barabara hili.

**OMBI KWA SERIKALI**

*Kasi ya ujenzi iongezeke kwa kuongezewa bajeti ya utekelezaji wa ujenzi wa barabara hili.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MENGINEYO

# (30 Juni 2023 – 1 Julai 2022)

# DHORUBA KUBWA NDANI YA ZIWA VICTORIA YAFANYA UHARIBIFU WA MITUMBWI NA NYAVU – TUNAOMBA MCHANGO WAKO

March 23, 2023



*Sehemu ya uharibifu uliofanyika kwenye Mwalo wa Kijiji cha Busekera, Kata ya Bukumi, Musoma Vijijini.*

Upepo wenye kasi kubwa na mvua kubwa vilisababisha kuwepo kwa dhoruba kubwa ndani ya Ziwa Victoria juzi tarehe 20.3.2023.

Mialo ya Musoma Vijijini ilikumbwa na dhoruba hiyo na uharibifu mkubwa umefanyika.

Tunaomba tushirikiane kuwachangia wavuvi wetu walioathirika na janga hili.

## TATHIMINI YA UHARIBIFU

**(1) Mitumbwi ya Mwalo wa Kijiji cha Busekera.**
*Iliyoharibika: 137
*Inayotengenezeka: 108
*Isiyotengenezeka: 29
*Makokoro ya dagaa yaliyoharibika: 29

**(2) Mitumbwi ya Mwalo wa Kijiji cha Buira.**
*Iliyoharibika: 39
*Inayotengenezeka: 29
*Isiyotengenezeka: 10
*Makokoro ya dagaa yaliyoharibiwa: 15

**(3) Mitumbwi ya Mwalo wa Kijiji cha Bwai Kumsoma.**
*Iliyoharibika: 25
*Inayotengenezeka: 21
*Isiyotengenezeka: 4
*Makokoro ya dagaa yaliyoharibika: 15

**(4) Mitumbwi ya Mwalo wa Kijiji cha Kasoma.**
*Iliyoharibika: 10
*Inayotengenezeka:9
*Isiyotengenezeka:1
*Makokoro ya dagaa yaliyoharibika: 3

## GHARAMA ZA MATENGENEZO

Mifano ya hapa chini itakupatia picha unayoweza kuitumia kutoa mchango wako.

(1) Gharama za kutengeneza Mtumbwi
*Tsh 1,700,000
*Ubao 1 wa 9"x10" unagharimu Tsh 12,000

(2) Gharama za kutengeneza Kokoro la Dagaa
*Tsh 1,400,000

**UWASILISHAJI WA MCHANGO WAKO**


**Tafadhali mpelekee:**
DC Wilaya ya Musoma
Simu: 0756 088 624

**Michango ya awali:**
*Tungalipenda kuanza kuwasilisha michango yetu ya awali kwa wavuvi waathirika siku ya Alhamisi, 30.3.2023

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# VIJANA WALIOENDA KUSOMA INDIA WAMSHUKURU PROF MUHONGO

September 20, 2022



*Vijana 6 waliopata ICCR scholarships za kusoma MSc in Applied Geology nchini India.*

Vijana sita (6) walioombewa ICCR scholarships na Prof Sospeter Muhongo kwenda kusoma India wamemshukuru Profesa huyo kwa kuwatafutia scholarships hizo.

Wanafunzi hao sita (6) walisoma MSc Applied Geology kwenye maeneo yafuatayo:

*Coal Geology
*Metamorphic Geology
*Mineralogy
*Mineral Processing

Prof Muhongo amepawa pongezi nyingi za kusoma na kufaulu masomo yao vizuri.

Vijana hao wote sita wanafanya kazi kwenye Taasisi za Serikali yetu.

**Shukrani kwa:**
Prof S Muhongo

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# PROF MUHONGO AMSAIDIA MAHITAJI YA SHULE KIJANA WA JIMBONI MWAKE AENDE KUANZA MASOMO YA KIDATO CHA V NYAKATO HIGH SCHOOL

August 31, 2022



*Msaidizi wa Mbunge, Vaileth Peter akiwa na kijana Jastine – wametoka Benki kufanya malipo ya shule, na tayari wamemaliza kununua vifaa vya shule, vikiwemo vitabu vinavyohitajika.*

Kijana Jastine Mgaya Bina wa Kijiji cha Kaburabura, Kata ya Bugoji alichelewa kuanza masomo ya Kidato cha Tano (Form V, HGL) kwa kukosa mahitaji ya shule.

Leo, kijana huyo amepata mahitaji yote ikiwemo nauli yake ya kwenda kuanza masomo yake Nyakato High School, Bukoba.

Picha iliyoambatanishwa hapa inamuonyesha Msaidizi wa Mbunge, Vaileth Peter akiwa na kijana Jastine – wametoka Benki kufanya malipo ya shule, na tayari wamemaliza kununua vifaa vya shule, vikiwemo vitabu vinavyohitajika.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KAMPENI YA SENSA MUSOMA VIJIJINI – KATA YA MAKOJO WAHAIDI KUHESABIWA KWA KIWANGO CHA ASILI MIA MOJA

August 16, 2022



*Hatua kubwa iliyofikiwa kwenye ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Makojo.*

Kata ya Makojo ina Vijiji 3 (Chimati, Chitare na Makojo) imemhaidi Mbunge wao wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo, kwamba wamejitayarisha kuhesabiwa wote, yaani kwa kiwango cha asili mia moja (100%).

Hiyo ahadi ilitolewa siku ya Jumamosi, tarehe 13.8.2022 wakati Mbunge huyo alipokuwa ndani ya Kata hiyo akifanya kampeni ya kushawishi Wanavijiji wa Kata hiyo (na Wageni wao) washiriki kwenye SENSA ya Watu na Makazi ya tarehe 23.8.2022.

Wakati wa majadiliano ya umuhimu wa kila kaya na kila mwananchi kuhesabiwa, Mbunge huyo aliwakumbusha Wana-Kata hiyo VIPAUMBELE vya MAENDELEO ya KATA yao (k.m. Elimu, Afya, Kilimo, Uvuvi) vinavyohitaji ushiriki na uchangiaji mkubwa wa Serikali yetu.

Viongozi wa Kata hiyo waliofuatana na Mbunge wa Jimbo kwenye Kampeni hii ni:
*Ndugu Peresi Mujaya (Mtendaji Kata, WEO)
*Ndugu Lameck Mtaki (Mtendaji wa Kijiji, VEO)
*Ndugu Daniel Magere (M/K Serikali ya Kijiji)

Miradi mikubwa ya Kata hii iliyokwishapata au inaendelea kupewa fedha kutoka Serikalini ni hii ifuatayo:

**Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Makojo**

Kata imeishapokea Tsh milioni 500 (Tsh 500m) kutoka Serikalini kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya.

Wanavijiji na Viongozi wao wanaishukuru sana Serikali kwa kuwapatia Mradi huu muhimu sana. Shukrani za kipekee ziende kwa Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan.

**Mradi wa Maji ya Bomba ya Ziwa Victoria**

Mradi huu wa thamani ya Tsh bilioni 1.072 (Tsh 1, 072m) ni wa kusambaza maji ya bomba kwenye Vijiji vya Chitare na Makojo.

Mradi ulianza kwenye Mwaka wa Fedha 2013/2014, ulisimamiwa na Halmashauri yetu na umechelewa kukamilika.

RUWASA inajitahidi kurekebisha kasoro zilizopo.

Wananchi wana imani kubwa na Serikali yetu ambayo itahakikisha Mradi huu unakamilika na maji safi na salama yanapatikana ndani ya Kata ya Makojo.

**Fedha za UVIKO- 19**

*Makojo Sekondari ilipewa Tsh milioni 60 (Tsh 60m) kujenga vyumba vipya 3 vya madarasa

*Shule Shikizi Mwikoko ilipewa Tsh milioni 60 (Tsh 60m) kujenga vyumba vipya 3 vya madarasa na ofisi 1. Shule hii tayari ilishapewa fedha za ujenzi wa vyumba vipya 2 vya madarasa na ofisi 1 kutoka Mradi wa Serikali wa EQUIP.

**Fedha za Mfuko wa Jimbo**

*Makojo Sekondari imegawiwa Mabati 158 na Saruji Mifuko 52 kutoka kwenye Fedha za Mfuko wa Jimbo zilizonunua (Mei 2022) vifaa vya ujenzi kwa Sekondari kadhaa za Jimboni mwetu.

**Miradi ya TARURA ndani ya Kata ya Makojo**

TARURA imekamilisha na inaendelea kuboresha barabara za eneo hili:

*Barabara ya Makojo- Chitare – Kurugee
*Barabara ya Chitare- Mwikoko Rusoli

Barabara hizi ni muhimu sana kwa uimarikaji wa uchumi wa wavuvi na wakulima wa eneo hili.

## BAADHI YA MIRADI MIPYA ILIYOPANGWA KUTEKELEZWA NDANI YA KATA YA MAKOJO

(1) Uvuvi wa Vizimba – wavuvi wako tayari kuanzisha vyama vya ushirika vya uvuvi kwa lengo la kupatiwa mikopo ya uvuvi wa vizimba.

(2) Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Chimati unaendelea.

(3) Makojo High School – Wanavijiji wamemuomba Mbunge wao ashirikiane nao kwenye ujenzi wa "High school" hiyo – Mbunge amekubali ombi hilo na kikao cha mradi huo kitafanyika mwishoni mwa Septemba 2022.

## UMUHIMU MKUBWA WA KUHESABIWA

Wanavijiji wa Kata ya Makojo wanao uelewa mkubwa wa umuhimu wa kuhesabiwa – wanakubali kwamba takwimu sahihi zinahitajika kwa mipango mizuri ya miradi yao ya maendeleo.

Kwa hiyo, Kata ya Makojo, kama zilivyo Kata nyingine 20 za Jimbo la Musoma Vijijini, WATAHESABIWA WOTE, yaani kwa asili mia moja (100%).

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## HITIMISHO

Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025 unaenda vizuri Jimboni mwetu, na mafanikio yake yanaonekana na kuthaminiwa sana na wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini. Wanavijiji wanashirikiana na Serikali yao ya ngazi mbalimbali kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo inayokidhi mahitaji ya jamii zao.

Taarifa hii ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Jimbo letu ni ya mwaka mmoja wa fedha, yaani 1 Julai 2022 hadi 30 Juni 2023. Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa Jimboni mwetu kwa kipindi hiki iliibuliwa kutoka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025), ambamo ndimo tulitoa vipaumbele vyetu vitano vya maendeleo.

Miradi yetu ya maendeleo ni endelevu, kwani inaibuliwa kutoka kwenye vipaumbele vyetu vitano ambavyo navyo ni endelevu, na nyenzo kuu za utekelezaji wake nazo zinaendelea kuhitajika kwa ustawi wa jamii yetu.

Vipaumbele vyetu ni: (i) elimu, (ii) afya, (iii) kilimo, uvuvi na ufugaji, (iv) tabianchi na mazingira, na (v) michezo na utamaduni.

Nyezo kuu zinazohitajika kwenye utekelezaji wa miradi ya vipaumbele vyetu ni maji, umeme, barabara, vyombo vya usafirishaji na mawasiliano, raslimali watu na taasisi za fedha na uchumi.

Ahadi zilizotolewa Jimboni mwetu na Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali yake, chini ya uongozi mzuri wa Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ziliendelea kutekelezwa ikiwemo ahadi ya ujenzi wa barabara la Musoma-Makojo-Busekera (km 92) kwa kiwango cha lami.

Ahadi za Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, zimetekelezwa na kuvuka malengo yaliyowekwa kwa mwaka huu mmoja (30 Juni 2023 - 1 Julai 2022). Michango ya Mbunge huyu ni mingi na mikubwa kama inavyoainishwa ndani ya kitabu hiki.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, anaendelea kushirikiana kwa ukaribu sana na wananchi, viongozi wa Chama (CCM) na wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye utekelezaji wenye mafanikio makubwa wa Ilani ya Uchaguzi (2020-2025) Jimboni mwao.

Vilevile, Mbunge huyu anaendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa shughuli za Chama chetu (CCM) kwa ngazi zote, yaani, kuanzia Matawi, Kata, Wilaya (Musoma Vijijini), Mkoa (Mara) hadi Taifa (Tanzania).

**SHUKRANI**

Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini na viongozi wao wa ngazi za Vitongoji (374), Vijiji (68) na Kata (21), na Mbunge wao wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, wanatoa shukrani nyingi za dhati kwa Mwenyekiti wa CCM Taifa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa uwezeshaji na uongozi wake mzuri kwenye utekelezaji wa miradi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja wa fedha (30 Juni 2023 - 1 Julai 2022).

Rais wa Serikali ya Mapinduizi ya Zanzibar na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Mhe Dkt Hussein Ali Mwinyi anapewa shukrani nyingi kwa ushauri wake mzuri anaoutoa kwenye utekelezaji wa miradi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya kipindi hiki cha mwaka mmoja wa fedha (30 Juni 2023 - 1 Julai 2022).

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt Philip Isdor Mpango anapewa shukrani nyingi kwa ushauri na ufuatiliaji mzuri anaoufanya kwenye miradi ya maendeleo ya Jimboni mwetu.

Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Mhe Dkt Ali Mohamed Shein, Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Mhe Abdulrahman Kinana, na Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Ndg Daniel Chongolo nao wanapewa shukrani nyingi za dhati kwa usimamizi wao mzuri wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu (CCM) kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja (30 Juni 2023 - 1 Julai 2022).

Waziri Mkuu, Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa, na viongozi wengine wote wa ngazi mbalimbali za Serikali yetu wanapewa shukrani nyingi za uwezeshaji na ushirikiano wao kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.

Kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja wa fedha (30 Juni 2023 - 1 Julai 2022). Utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Jimboni mwetu) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ulisimamiwa vizuri ki-Serikali na Wakuu wawili wa Mkoa wa Mara wa wakati huo ambao ni Mhe Ally Hapi na Mhe Meja Jenerali Suleiman Mzee.

Mkuu wa Wilaya yetu ya Musoma, Mhe Dkt Khalfany Boniface Haule anapongezwa na kupewa shukrani nyingi za dhati kwa uchapaji kazi wake mzuri wenye ufuatialiji na usimamiaji makini wa miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa Jimboni mwetu.

Shukrani nyingi pia zinatolewa kwa viongozi mbalimbali wa Chama cha Mapinduzi na Jumuiya zake kuanzia ngazi za Tawi, Kata, Wilaya hadi Mkoa (Mara). Baadhi yao ni Mlezi wa Mkoa ki-Chama, Ndugu Abdulrahman Kinana, M-NEC Mkoa, Ndugu Christopher Gachuma, Mwenyekiti wa Mkoa, Ndugu Patrick Chandi Marwa, Katibu wa Mkoa, Ndugu Langaeli Akyoo. Wengine ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Musoma Vijijini, Ndugu Denis Ekwabi na Katibu wa Chama Wilaya, Ndugu Noverty Bathromeo Kibaji.

Waheshimiwa Madiwani wote 28 wakiwemo wa Viti Maalumu, na wafanyakazi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (Musoma DC) wanapewa shukrani za dhati kwa utimizaji wa wajibu wao kwenye utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu (CCM) ndani ya mwaka huu mmoja.

Shukrani nyingi inapewa RUWASA kwa kufufua miradi iliyokwama kwa miaka kadhaa, na kuanza utekelezaji wa miradi mipya ya usambazaji wa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria, na uchimbaji wa visima virefu vya maji vijijini mwetu.

TARURA na TANROADS wanaendelea kuboresha barabara zetu ambazo zinapitika kwa urahisi kwa majira yote ya mwaka.

Vyanzo vya fedha na vifaa vya utekelezaji wa miradi ya maendeleo vijijini mwetu iliyobuniwa kutoka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025) ndani ya mwaka huu mmoja wa fedha (30 Juni 2023 - 1 Julai 2022), ni vingi vikiwemo: Serikali Kuu na miradi yake kama vile EQUIP, EP4R, Wadau wa Maendeleo (PCI Tanzania na BMZ Germany), Benki za NBC, NMB na CRDB.

Mbunge wa Jimbo ametoa michango mingi na mikubwa kuchangia utekelezaji wa miradi inayoelezwa ndani ya kitabu hiki. Wanavijiji wamechangia nguvukazi na fedha taslimu. Baadhi ya Wazaliwa wa Musoma Vijijini wametoa michango yao na majina yao yametajwa ndani ya kitabu hiki. Michango kutoka kwa Wadau wengine wa Maendeleo ya Jimboni mwetu imeainishwa ndani ya kitabu hiki.

Mbunge wa Jimbo anapenda kuwashukuru watu mbalimbali wenye fani mbalimbali anaofanya nao kazi za Jimbo la Musoma Vijijini. Orodha ni ndefu na kwa uwakilishi wao anamshukuru Mtendaji Mkuu (Webmaster) wa Tovuti ya Jimbo letu (www.musomavijijini.or.tz), Dkt Isack Kambira.

Wengine wanaopewa shukrani ni Waandishi wa Habari wakiwakilishwa na Ndugu Sadick Hunga, Mussa Makali na Shomari Binda. Wafanyakazi wa Ofisi ya Mbunge wanapewa shukrani nyingi kwa kazi zao nzuri - hao ni Vaileth Peter, Benjamin John na Abdallah Juma.

Shukrani za kipekee na za muhimu sana zinapewa WANANCHI wa Jimbo la Musoma Vijijini ambao kwa utashi wao wenyewe wameamua kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025. Miradi ya maendeleo inayotekelezwa vijijini mwao inabuniwa, inachangiwa (nguvukazi na fedha tasilimu), inatekelezwa na inatunzwa na wao wenyewe.

Vilevile, wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanashirikana vizuri sana na Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa manufaa makubwa ya ukuaji, uimarikaji wa uchumi na ustawi wa Jimbo letu la Musoma Vijijini.

**Kitabu hiki kimetayarishwa na:**
Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini


**Prof. Dr.rer.nat. Sospeter M Muhongo**
Officier, Ordre des Palmes académiques
FGSAf, FAAS, MASSAf, FASI, FASSAf, FTAAS, FGIGE,
FTWAS, HonRFCAGS, HonFGSA, HonFGS, CGeol, EurGeol

**Homepage/Tovuti:**
www.musomavijijini.or.tz

**Telephone/Simu:**
+255 754 400 800



**Date/Tarehe:**
30 Juni 2023